



## Dosari za Kifonolojia Zinazojitokeza kwa Wangoni Wanapojifunza Kiswahili

Arnold Gawasike Msigwa<sup>1</sup>, Edward Shanel Nyoni<sup>2</sup>

<sup>1</sup>Taasisi ya Taaluma za Lugha, Chuo Kikuu cha Kabale

<sup>2</sup>Shule ya Sekondari Bukamage, Muleba, Kagera

Corresponding author: [agmsigwa@kab.ac.ug](mailto:agmsigwa@kab.ac.ug)

### Article History:

**Received:** 7 Mar 2025

**Accepted:** 23 Oct 2025

**Published:** 26 Dec 2025

### Maneno Muhimu:

Dosari, kifonolojia,  
Kiswahili, Wangoni

*This is an open access article  
under the CC-BY-NC-ND license*



### IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza dosari za kifonolojia zinazojitokeza kwa jamii ya Wangoni wanapojifunza Kiswahili. Tatizo la utafiti lilichochoewa na watafiti wengi kutafiti dosari kwa Wabantu wanapojifunza lugha ya pili yenye mfumo tofauti na lugha yao ya kwanza. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Dosari ya Corder (1967) inayoeleza kwamba dosari katika ujifunzaji wa lugha ya pili hazitokani tu na mifumo tofauti kati ya lugha ya kwanza na lugha ya pili, bali kuna masuala anuwai mengine yanayomzunguka mjifunzaji na kuchangia kuibuka kwa dosari. Utafiti ulikusanya data katika wilaya ya Songea vijijini katika shule za sekondari Nalima na Liganga. Utafiti ulihusisha jumla ya watoataarifa 24 ambao ni wanafunzi wanaosoma kidato cha tatu pamoja na walimu wanaofundisha Kiswahili katika shule hizo. Mbinu zilizotumika kukusanya data ni majadiliano ya kundi na hojaji. Uchambuzi wa data za utafiti huu umetumia mbinu ya maelezo ambapo dosari zote zilizobainika ziliwekwa katika makundi maalum na kutolewa maelezo kikamilifu. Matokeo yanaonesha kwamba zipo dosari za kifonolojia zinazojitokeza kwa Wangoni wanapojifunza Kiswahili, hususani upachikaji wa sauti, mfano neno, afurika, sauti /u/ inapachikwa ubadilishaji wa sauti, mfano miladi badala ya 'miradi' na udondoshaji, mfano neno akuna badala ya 'hakuna'. Ili kuwafanya wajifunzaji hawa wajifunze Kiswahili kwa usahihi, ilipendekezwa kuwa, kuwepo na mchanganyiko wa wanafunzi kutoka ndani na nje ya mkoa katika shule za kata, kuwepo kwa midahalo, makongamano na majarida ya Kiswahili ya kutosha, pia yafanyike mazoezi shirikishi kwa shule zaidi ya moja.

## Abstract

*This study investigates phonological manifestations among the Ngoni community learning Kiswahili as a second language. The study was motivated by previous research that focused mainly on Bantu communities learning structurally different second languages, while overlooking errors committed by learners whose first languages are closely related to Kiswahili. The study was guided by Corder's (1967) Error Analysis Theory and its later modifications, which posit that errors committed by second language learners are not only caused by linguistic differences between languages, but also by other contributing factors. The study was conducted in rural Songea District, Tanzania, specifically at Nalima and Liganga Secondary Schools. The study population comprised Kiswahili teachers and secondary school students, from whom 24 Form Three students and Kiswahili teachers were selected as the sample. Data were collected through questionnaires and focus group discussions. Descriptive data analysis was employed, whereby identified data were organized into categories based on similarities and variations, followed by detailed descriptions. The results indicate that the major phonological errors manifested among Ngoni learners of Kiswahili include sound insertion, such as the insertion of the vowel /u/ in the word afurika; sound deletion, such as akuna instead of hakuna (deletion of the sound /h/); and sound substitution, such as samana instead of thamanna (substitution of the sound /θ/). Based on these findings, the study recommends the establishment of mixed-ethnicity student populations in ward schools, the promotion of Kiswahili debates among students, and the organization of Kiswahili symposiums. Finally, the study emphasizes the importance of integrative speaking practices among neighbouring schools to enhance Kiswahili speaking competence among students.*

**Key Words:** Error, Phonology, Kiswahili, Ngoni

### 1.1 Usuli na Utangulizi

Suala la chanzo cha dosari zinazojitokeza miongoni mwa wajifunzaji wa lugha ya pili (kuanzia sasa Lg2) limekuwa na mjadala changamani miongoni mwa wataalamu. Kwa mfano, Lado (1957) akijadili kuhusu Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi anadai kwamba chanzo kikubwa cha dosari zinazo jitokeza kwa wajifunzaji wa Lg2 ni utofauti wa mifumo ya lugha ya kwanza (kuanzia sasa (Lg1) na Lg2. Tofauti ya mifumo hiyo, yaani Lg1 na Lg2 husababisha athari kadhaa kwa Lg2 wanayojifunza na hivyo dosari hujitokeza kwa wingi. Suala hili lilisababisha watafiti kama (taz, Mudhune, 2008 na Ontieri, 2013) kuchunguza zaidi dosari katika lugha zenye mifumo inayotofautiana. Kwa mujibu wa wataalamu hawa kutofautiana kwa mifumo ya lugha hizo ndizo sababu kiini za dosari zinazojitokeza kwa Wabantu wanapojifunza Kiswahili.

Mawazo ya Lado (1957) yanakinzana na Corder (1967), ambaye kupitia Nadharia ya Uchanganuzi Dosari anadai kwamba dosari katika ujifunzaji wa Lg2 hazitokani tu na tofauti ya mifumo kati ya Lg1 na Lg2 ambayo mjifunzaji anajifunza. Hoja kuu ya mtaalamu huyu ni kwamba yako mambo mengine yanayoweza kusababisha utokeaji wa dosari, kama vile jinsi mjifunzaji wa lugha anavyoielewa hiyo Lg2, mbinu anazotumia mjifunzaji kujifunza lugha hiyo, na hata matatizo au changamoto anazokabiliana nazo wakati wa kujifunza lugha husika. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uchanganuzi Dosari, mambo hayo yaliyojadiliwa yanaweza kusababisha dosari nyingi kwa wajifunzaji wa Lg2 hata kama lugha hizo zina mifumo inayofanana. Aidha, Nyanda (2015) akielekea kuungana na Corder (keshatajwa) anafafanua kwamba, miongoni mwa sababu zinazosababisha utokeaji wa dosari kwa wajifunzaji wa Lg2 ni pamoja na wajifunzaji wenyewe kutoweka jitihada katika ujifunzaji wa lugha hiyo, kukosekana kwa msamiati wa lugha wanayojifunza na mazingira duni ya ujifunzaji wa Lg2.

Kadhalika, Mbula (2011) alifafanua kwamba chanzo cha dosari kwa wajifunzaji wa Lg2 ni tofauti wa mifumo ya kiisimu ya Lg1 na Lg2 wanayojifunza. Kulingana na Mbula (keshatajwa) mifumo ya Lg1 dhidi ya ile ya Lg2 inapotofautiana inasababisha ugumu katika mchakato wa kujifunza lugha husika. Kutokana na hali hii utokeaji wa dosari huwa ni wa kiwango cha juu, lakini Dulay na Burt (1974) wanadai kwamba katika ujifunzaji wa Lg2, kigezo cha mpishano wa mifumo ya Lg1 dhidi ya ile ya Lg2 si kigezo faafu cha utokeaji wa dosari kwa wajifunzaji wa Lg2, bali mazingira yote yanayowazunguka wajifunzaji yana nafasi ya kuwa chanzo cha dosari.

Kuhusu hali ya lugha ya Kiswahili katika eneo la utafiti na nchini Tanzania kwa ujumla. Kiswahili ni Lg2 kwa wazungumzaji wengi wa Kibantu hasa wale wanaopatikana katika mazingira ya vijijini kama ilivyo kwa Wangoni. Watanzania walio wengi wanaozaliwa katika mazingira ya vijijini, wanazo Lg1 ambazo ndizo huanza kuziamili na kuzitumia mara baada ya kuzaliwa tu. Wangoni kama ilivyo kwa Watanzania walio wengine, nao wanaangukia katika sifa hizo. Uchunguzi uliofanywa na watafiti mbalimbali kama vile Gawasike (2016) na Msigwa na Vavayo (2020) unaonesha kwamba, watoto wengi wa kijijini nchini Tanzania huanza kujifunza Kiswahili pale wanapoanza shule za msingi; wakiwa na umri wa miaka kati ya 6 na 7 ambao ndiyo umri wa kisheria wa kuanza shule za msingi. Katika umri huo, mifumo ya Lg1 huwa inakuwa imejengeka na kuimarika kiasi kwamba, huwawia vigumu kuanza kuingiza mifumo mingine mipya. Wakiegemeza hoja zao

katika Nadhariatete ya Kipindi Faafu<sup>1</sup> wanaonesha kuwa muda faafu wa kuamili na kumuda lugha unakuwa umeshapita. Hivyo, changamoto za uingizaji wa lugha mpya haukwepeki. Kwa mfano, utafiti wa Msigwa na Vavayo (2020) unadhihirisha hali hiyo. Utafiti huu ulihusu dosari za kifonolojia zinazojitokeza kwa Wamasai wanapojifunza Kiswahili kama Lg2.

Kwa kuwa, lugha nyingi za Kibantu zina mifumo inayofanana, yawezekana ndio maana tafiti kuhusu utokeaji wa dosari kwa Wabantu wanaojifunza Kiswahili hazijafanyika vya kutosha kwa sababu wataalamu inaelekea wanaamini kwamba lugha hizo zenye mifumo inayofanana dosari haziwezi kujitokeza kwa wingi wakati wazungumzaji wa lugha za Kibantu wakijifunza lugha hizo hususani Kiswahili. Kukosekana kwa tafiti za namna hii kunasababisha wataalamu na watafiti wengi kushughulikia dosari zinazojitokeza kwa wajifunzaji wa lugha za Kibantu ambazo zina mifumo inayotofautiana. Kwa hiyo, utafiti huu ulilenga kubainisha dosari za kifonolojia zinazojitokeza kwa Wangoni wanapojifunza Kiswahili.

### **1.2 Tatizo la Utafiti**

Tafiti za hivi karibuni (Taz, Virginia, 2016; Kiswakwa: 2014) zilichanganua dosari za kifonolojia zinazojitokeza kwa wazungumzaji wa lugha za Kibantu wanapojifunza Kiswahili sanifu. Katika tafiti zao wamejikita kuchunguza lugha za Kibantu zenye miundo tofauti na kubainisha dosari nyingi zinasababishwa na utofauti wa miundo ya lugha hizo. Tafiti kuhusiana na dosari zinazojitokeza kwa wazungumzaji wa lugha za Kibantu yaani Kiswahili na Kingoni zenye miundo inayofanana hazijafanyika vya kutosha. Hii ni kwa sababu wataalamu wamejikita zaidi kuchunguza dosari kwa wajifunzaji wa lugha zenye miundo inayotofautiana.

### **1.3 Malengo ya Utafiti**

Makala haya, yalilenga kubainisha dosari za kifonolojia zinazojitokeza kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wangoni.

## **2.0 Mapitio ya Maandiko na Kiunzi cha Nadharia**

Maandiko ya wataalamu na watafiti mbalimbali yalitumika katika kufanikisha makala hii. Kadhalika, utafiti wa makala hii ulitumia Nadhari ya Uchanganuzi Dosari iliyoasisiwa na Corder (1967).

### **2.1 Dosari za Kifonolojia kwa Mujibu wa Tafiti Tangulizi**

Al-Shuabi (2006) alifanya uchanganuzi wa dosari za kifonolojia kwa Wayemeni

---

<sup>1</sup> Nadhariatete ya Kipindi Faafu ni tafsiri ya Kiingereza ya Nadhariatete ya Critical Period Hypothesis

wanaojifunza Kiingereza ikiwa ni lugha ya pili. Matokeo ya uchanganuzi wake yalibaini kuwepo kwa dosari za upachikaji wa sauti ya irabu katika silabi yenye mfuatano wa konsonanti tatu. Pia, alibaini udondoshaji wa sauti mwishoni mwa maneno ya lugha ya Kiingereza. Vilevile, mtafiti alifafanua kwamba dosari nyingi zilizojitokeza zilitokana na miundo tofauti ya lugha hizo zilizokuwa zikitumika na Wayemeni waliokuwa wakijifunza Kingereza. Utafiti wa Al-Shuabi ni tofauti na utafiti huu, kwa sababu utafiti huu utachunguza dosari za Kifonolojia kwa Wangoni wanaojifunza Kiswahili ikiwa ni lugha ya pili. Kadhalika, lugha ya Kingoni na Kiswahili ni lugha zenye miundo inayofanana.

Amro (2013) alifanya uchanganuzi wa dosari za kimatamshi kwa wazungumzaji wa lugha ya Kiarabu wanapojifunza Kiswahili ikiwa ni lugha yao ya pili katika chuo kikuu cha British, Dubai. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kuwepo kwa dosari mbalimbali zikiwemo dosari za uchopekaji wa sauti mwishoni mwa silabi katika maneno. Utafiti wa Amro (keshatajwa) ni tofauti na utafiti huu, kwa sababu, utafiti huu ulishughulikia dosari za kifonolojia kwa Wangoni wanapojifunza Kiswahili. Sampuli ya utafiti iliyotumika katika utafiti huu ni wanafunzi wanaosoma kidato cha tatu katika shule mbili za sekondari. Vilevile utafiti huu ulichunguza dosari zinazojitokeza kwa wajifunzaji ambao lugha yao ya kwanza ina uhusiano wa kiisimu na lugha ya pili wanayojifunza. Utafiti wa Arnaud (2015) umeshughulikia dosari za kifonolojia kwa Wangoni wanapojifunza Kiswahili. Vilevile, utafiti huu umeshughulikia dosari kwa wajifunzaji wa lugha zenye mifumo na miundo ya kiisimu inayofanana.

Badawi (2012) alifanya uchanganuzi wa dosari za Kifonetiki, kimofolojia na kisintaksia zinazojitokeza kwa wanafunzi wanaozungumza lugha ya Kiarabu wanapojifunza Kingereza kutoka katika Chuo Kikuu cha King Khalid, Saudi Arabia. Matokeo ya uchanganuzi wake yalibaini kuwepo kwa dosari mbalimbali kulingana na eneo lililoshughulikiwa. Katika uchanganuzi wa dosari za kifonetiki, mtafiti alibaini dosari kwa wajifunzaji hao hususani kuongeza sifa ya mkazo katika silabi na kuondoa sifa ya mkazo katika silabi. Vilevile, mtafiti alibaini dosari za ubadilishaji wa sauti katika maneno mbalimbali, matumizi ya sauti /ə/ badala ya sauti/ɔ/, pia, matumizi ya sauti /ə/ badala ya /ɔ/. badawi (keshatajwa) alichunguza dosari kwa wajifunzaji wa lugha zenye miundo na mifumo tofauti ya kiisimu. Hivyo utafiti huo, ni tofauti na utafiti huu, kwani ulichunguza dosari za kifonolojia kwa Wangoni wanapojifunza Kiswahili. Lugha ya Kingoni na lugha ya Kiswahili ni lugha zenye uhusiano wa karibu na mifumo inayofanana.

Arnaud (2015) alifanya uchunguzi wa matatizo ya utamkaji wa maneno kwa wanafunzi wa Kitanzania wanapojifunza lugha ya Kifaransa katika chuo kikuu cha Tlemcen. Sampuli ya utafiti wake ilihusisha wanafunzi wa kitanzania 20 wanaosoma katika chuo kikuu cha Tlemcen. Wanafunzi 15 walikuwa ni wa jinsia ya kiume na wanafunzi 05 walikuwa ni wa jinsia ya kike. Matokeo ya uchunguzi wake yalibainisha kwamba, wanafunzi hao walipata changamoto kutamkaa baadhi ya sauti zilizopo katika lugha ya Kifaransa kama vile sauti /R/ and /oe/, vilevile walishindwa kutamka kwa ufasaha sauti /ʔ /, /y/, /o/, /ø/, /ə/, /oe / na sauti /ɑ/ na /α / . Kulingana na matokeo ya uchunguzi huo, wanafunzi walikuwa wakitamka sauti hizo kwa kuzirudiarudia mara nyingi kutokana na kushindwa kuzitamka kwa ufasaha. Utafiti wa Arnaud (2015) ni tofauti na utafiti huu, kwa kuwa utafiti umeshughulikia dosari za kifonolojia kwa Wangoni wanapojifunza Kiswahili. Vilevile, utafiti huu umeshughulikia dosari kwa wajifunzaji wa lugha zenye mifumo na miundo ya kiisimu inayofanana.

## 2.2 Kiunzi cha Nadharia

Makala hii iliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Dosari. Nadharia hii iliasisiwa na Corder (1967). Nadharia hii ilianzishwa kama mbadala wa Nadharia ya Usasanyuzi Linganishi iliyoshindwa kuelezea aina zote za dosari ambazo zinaweza kufanywa na wajifunzaji wa lugha ya pili. Nadharia ya Uchanganuzi Dosari inaeleza kuwa dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha ya pili zinatokana na vyanzo mbalimbali kama vile mwingiliano uliopo ndani ya lugha ya pili, ujumlishaji mno wa kanuni za lugha ya pili wanayojifunza, ufundishaji usio sahihi, jinsi mjifunzaji wa lugha ya pili anavyoielewa lugha hiyo, mbinu anazozitumia kujifunza lugha hiyo na changamoto anazokutana nazo. Kwa hiyo, msingi mkuu wa nadharia hii ni kwamba dosari nyingi za wajifunzaji wa lugha ya pili zinatokana na wajifunzaji wenyewe kutumia kimakosa kanuni za lugha ya pili. Mtazamo wa nadharia hii unaungwa mkono na Dulay na Burt (1974) ambao katika utafiti wao wanaeleza kuwa mwingiliano wa lugha ya kwanza na uundaji wa tabia sio kipimo pekee cha kusababisha utokeaji wa dosari kwa wajifunzaji wa lugha ya pili, bali yapo mambo mengine kama vile mchakato wa ujifunzaji wa lugha na jitihada binafsi za wajifunzaji wenyewe. Makala hii ilitumia hatua tano zinazopendekezwa na Corder (1967) kupitia nadharia hii. Hatua ya kwanza ni kutafuta na kukusanya sampuli wajifunzaji wepi? wa kiwango gani?; pili, ni kutambua na kubaini dosari, hatua ya tatu ni kueleza dosari, hatua ya nne ni kufafanua dosari na hatua ya tano ni kutathmini dosari hizo. Kutokana na ufafanuzi wa nadharia hii, mtafiti alitumia nadharia hii kama mwongozo wa kushughulikia dosari zinavyojitokeza kwa Wangoni wanapojifunza Kiswahili pamoja na chanzo cha dosari hizo kwa kuhusisha

na namna nadharia inavyozingatia sababu za utokeaji wa dosari hizo.

### 3.0 Mbinu za Utafiti

Data za makala hii zilikusanywa kutoka wilaya ya Songea katika kata za Liganga na Litisha zilizopo mkoani Ruvuma. Uteuzi wa kata hizo unatokana ukweli kwamba, maeneo hayo ni miongoni mwa maeneo ambayo hayana mwingiliano mkubwa na jamiilugha nyingine kama Kimatengo, Kindendeule, na Kinyasa; hii ni kwa mujibu wa Mapunda (2016). Data hizo zilikusanywa uwandani Februari, 2020 ambapo mbinu ya majadiliano ya kundi ilitumika. Katika mbinu hii, watoataarifa walipewa nafasi ya kufanya majadiliano ya mada iliyohusiana na “ usafi wa mazingira” kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Sampuli ya watoataarifa ilikuwa jumla ya wanafunzi 20 wazungumzaji wa lugha ya Kingoni wanaosoma katika shule za sekondari Liganga na shule ya sekondari Litisha. Watoa taarifa hao ambao ni wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili walihusika katika utafiti huu kwa kufanya majadiliano ya kundi yaliyosaidia kupata data za kuhusiana na dosari za kifonolojia zilizojitokeza miongoni mwao.

### 4.0 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Uwasilishaji wa data za makala hii unahusu kuchunguza dosari zinazojitokeza kwa Wangoni wanapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

#### 4.1 Dosari za Kifonolojia Zinazojitokeza kwa Wangoni wanapojifunza Kiswahili

Lengo la kwanza la utafiti katika makala hii lilikuwa ni kubainisha dosari mbalimbali za kifonolojia zinazojitokeza kwa wanafunzi wa Kingoni wanapojifunza Kiswahili. Katika kubaini dosari hizo mtafiti alitumia mbinu ya majadiliano ya vikundi. Majadiliano ya vikundi yaliwahusisha wanafunzi wa kidato cha tatu ambao ni wazungumzaji wa lugha ya Kingoni. Utafiti ulitaka kubaini, *Je, ni dosari zipi za kifonolojia zinazojitokeza kwa Wangoni wanapojifunza Kiswahili?* Kutokana na swali hilo, matokeo ni kama yalivyobainishwa katika jedwali Na 1.1.

#### Jedwali Na. 1.1 Aina ya Dosari zinazojitokeza miongoni mwa Wajifunzaji Lugha

Na.	Aina ya Dosari	Mfano wa Dosari
i.	Dosari za upachikaji	afurika, asikari, watupage
ii.	Ubadilishaji wa sauti	gala, garimu, yenyewe
iii.	Dosari za Udondoshaji	akuna, talee, aki, asubui

## Chanzo: Data za Uwandani

Kwa ujumla utafiti huu umebainisha makundi ya aina tatu ya dosari zinazojitokeza miongoni mwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wagoni; ambazo ni dosari za upachikaji wa sauti. Yaani kuingiza sauti katika mazingira ambapo sauti hiyo haitarajiwi kuwapo kwa mujibu wa kanuni sa Kiswahili sanifu. Pili, ni ubadilishaji wa sauti, yaani kuingiliana kwa sauti katika mazingira ya utamkaji ambao unaelekea kujitokeza mpaka katika maandishi. Na mwisho ni dosari za udondoshaji, yaani kuondoa sauti fulani katika mazingira ambamo sauti hiyo haitarajiwi kuondolewa kwa mujibu wa Kiswahili Sanifu. Ufafanuzi na mifano mahsusi ya dosari hizi unafanyika katika sehemu zinazofuata hapa chini.

### 4.1.1 Dosari za Upachikaji wa Sauti na Silabi

Kwa mujibu wa Massamba (2016:41) upachikaji ni utaratibu wa kuongeza kipashio cha kiisimu katika silabi, neno, kirai au kishazi. Upachikaji unaweza kufanyika kuanzia kiwango cha sauti mpaka kiwango cha sentensi. Massamba anasema kwamba mfuatano wa sauti za aina moja kama vile konsonanti na konsonanti au irabu na irabu haupendelewi sana katika utamkaji wa maneno hususani miongoni mwa wazungumzaji wa lugha za Kibantu. Mara nyingi silabi zenye mfuatano wa konsonanti na konsonanti hupachikwa vokali ili kuzuia konsonanti kufuatana. Wanafunzi wa Kingoni walibainika kupachika baadhi ya sauti katika maneno, hivyo kusababisha maneno hayo kuwa na dosari. Jedwali Na. 1.2 chini linadhihirisha hali hiyo:

**Jedwali Na. 1.2: Dosari za Upachikaji Kiswahili Sanifu Wa Irabu**

Na.	Dosari	Kiswahili Sanifu
a)	<i>Afirika</i>	<i>Afrika</i>
b)	<i>asikirimu</i>	<i>askrimu</i>
c)	<i>asikari</i>	<i>askari</i>
d)	<i>Afurika</i>	<i>Afrika</i>
e)	<i>Alufajiri</i>	<i>alfajiri</i>

## Chanzo: Data za Uwandani

Katika Jedwali Na. 1.2 data a-e imebainika kwamba irabu /i/ inapachikwa katika silabi yenye muundo wa KKI kwa lengo la kupata muundo wa silabi wa KI ili kurahisisha matamshi. Kadhalika, katika mfano wa dosari namba 1 (d) na (e) irabu/u/ ilipachikwa katika neno *alfajiri* na *Afrika* ili kuvunja mkururo wa silabi wenye muundo wa Konsonanti+ konsonanti na irabu ambao unawapa changamoto katika kutamka maneno ya namna hiyo. Matokeo ya namna hii pia yaligundulika na

Nyagah (2016) ambaye alibaini wazungumzaji wazawa wa Lugha ya Kimeru nchini Kenya walifanya dosari za upachikaji wa sauti wakati wakizungumza lugha ya Kiswahili. Kulingana na Nyagah (ameshatajwa) upachikaji huo ulifanywa ili kurahisisha utamkaji wa maneno husika kwa kuvunja mkururo wa Konsonanti+konsonanti+ Irabu ambao umekuwa ukiwasumbua wazungumzaji wengi wa lugha za Kibantu. Kulingana na Nadharia ya Uchanganuzi Dosari, wajifunzaji wa lugha ya pili wanatumia miundo ya lugha ya kwanza kwenye lugha ya pili na hivyo kusababisha utokeaji wa dosari wakati lugha ya pili inapotumika. Utafiti pia ulibaini watoataarifa walifanya dosari kwa kupachika silabi \$ga\$, \$ge\$ na \$gi\$ mwishoni mwa maneno wakati wa utamkaji wa maneno ya Kiswahili. Upachikaji wa silabi hizo umesababisha maneno husika kutamkwa kimakosa na hivyo kusababisha kuwepo kwa dosari hizo. Licha ya kwamba silabi hizo zina athari kimofolojia lakini pia zimeleta athari za kifonolojia na kusababisha dosari. Dosari hizo zinabainika kupitia Jedwali Na. 1.3 hapa chini: Upachikaji wa Silabi \$ga\$, \$ge\$ na \$gi\$

**Jedwali Na. 1.3: Upachikaji wa Silabi \$ga\$, \$ge\$ na \$gi\$**

Na.	Dosari	Kiswahili Sanifu
a)	<i>sijuagi</i>	<i>sijui</i>
b)	<i>tunafanyaga</i>	<i>huwa tunafanya</i>
c)	<i>wafanyage</i>	<i>wafanye</i>
d)	<i>watupage</i>	<i>watupe</i>
e)	<i>hawajagi</i>	<i>huwa hawaji</i>

**Chanzo:** Data za Uwandani

Katika mfano kutoka katika jedwali Na. 1.3 mfano wa (a) - (e) silabi \$ga\$, \$ge\$ na \$gi\$ zilipachikwa katika maneno husika na hivyo kusababisha utamkaji wenye dosari. Dosari hii imetokana na ukweli kwamba watoataarifa hawa walipachika silabi hizo katika maneno zikilenga kuwa mbadala wa kitenzi cha hali ya mazoea cha *huwa*. Dosari hizo za kupachika viambishi katika maneno ya lugha ya Kiswahili zinadhihirisha kwamba wanafunzi hao bado hawajamudu vizuri lugha ya Kiswahili na hivyo kutamka maneno kimakosa.

Suala la dosari za upachikaji wa silabi linashadidiwa na Nadharia ya Uchanganuzi Dosari inayoeleza kwamba miongoni mwa dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha ya pili ni dosari zinazohusu upachikaji wa vitamkwa mbalimbali kama vile sauti, silabi na viambishi mbalimbali katika lugha wanayojifunza.

#### 4.1.2 Dosari za Ubadilishaji wa Sauti

Mtafiti alibaini kwamba watoataarifa wa jamii ya Kingoni walitumia sauti mbadala mahali pasipostahili na hivyo kusababisha dosari katika matamshi. Sauti zilizotumiwa kama mbadala wa sauti ya awali zilisababisha maana ya neno husika kutokuwa sahihi. Dosari nyingi katika maneno husika zilijibainisha mwanzoni mwa neno. Data katika jedwali Na. 1.4 zinadhihirisha hali hiyo.

**Jedwali Na. 1.4: Dosari za Ubadilishaji wa Sauti**

Na.	Mfano wa Dosari	Kiswahili Sanifu
a)	<i>Garimu</i>	<i>gharimu</i>
b)	<i>gali</i>	<i>ghali</i>
c)	<i>gala</i>	<i>ghala</i>
d)	<i>galama</i>	<i>gharama</i>
e)	<i>gafla</i>	<i>ghafla</i>

**Chanzo:** Data za Uwandani

Kama mifano ya data kutoka katika Jedwali Na. 1.4 inabainisha kwamba wanafunzi wa jamii ya Kingoni walifanya dosari katika kutumia sauti /g/ badala ya sauti /ɣ/ wakati wa kutamka maneno yenye sauti inayoanzia na /ɣ/. Uchanganyaji wa sauti hizo ulisababisha watamke maneno hayo kimakosa na hivyo kusababisha dosari ambapo sauti /ɣ/haimo kwenye mfumo wa sauti za Kingoni hivyo, sauti /g/ ambayo pia hutamkiwa kwenye kaakaa laini huchukua nafasi ya sauti /ɣ/. Sauti hizo mbili hutamkiwa kwenye sehemu sawa ya kinywa ingawa moja ni kipasuo ilhali nyingine ni kikwamizwa. Jedwali Na. 1.5 hapa chini linadhihirisha mfano wa dosari hizo za ubadilishaji wa sauti

**Jedwali Na. 1.5: Dosari za Ubadilishaji wa Sauti /ð/ na /θ/**

Na.	Dosari	Kiswahili Sanifu
a)	<i>zibiti</i>	<i>dhibiti</i>
b)	<i>baazi</i>	<i>baadhi</i>
c)	<i>zibitisha</i>	<i>thibitisha</i>
d)	<i>mazala</i>	<i>madhara</i>
e)	<i>asari</i>	<i>athari</i>

**Chanzo:** Data za Uwandani

Vilevile, katika mfano kutoka kwenye jedwali Na.1.5(a) – (e) wanafunzi wa jamii ya Kingoni walidondosha sauti /ð/ na /θ/ wakati wa mazungumzo na hivyo sauti nyingine badala yake zikatumika. Nafasi ya sauti /ð/ ilikaliwa na sauti /z/ wakati katika nafasi ya sauti /θ/ ilipachikwa sauti /s/. Mfano wa dosari za ubadilishaji wa sauti ni kama vile *baazi* badala ya *baadhi*, *kuzibiti* badala ya *kudhibiti*, *asari* badala

ya athari. Sababu kubwa ya kuichagua sauti /s/ ambayo pia ipo kwenye orodha ya fonimu za lugha ya Kingonini kwamba inakaribiana zaidi na /θ/ na kwamba zote ni vikwamizwa ghuna. Jedwali Na. 1.6 linaonesha dosari za ubadilishaji wa sauti /r/.

**Jedwali Na. 1.6: Dosari za Ubadilishaji wa Sauti /r/**

Na.	Dosari	Kiswahili Sanifu
a)	<i>kukabilia</i>	<i>kukabiriana</i>
b)	<i>amli</i>	<i>amri</i>
c)	<i>selikali</i>	<i>serikali</i>
d)	<i>tulilipoti</i>	<i>tuliripoti</i>
e)	<i>miladi</i>	<i>miradi</i>

**Chanzo:** Data za Uwandani

Data katika jedwali Na. 1.6 (a) – (e) wanafunzi walifanya ubadilishaji wa sauti ambapo mahali palipotakiwa kuwepo sauti /r/ waliweka sauti /l/ kama mbadala wake na hivyo kusababisha utamkaji usio sahihi wa maneno kama vile, *miladi* badala ya ‘miradi’, *tulilipoti* badala ya ‘tuliripoti’ na *selikali* badala ya ‘serikali’. Ontieri (2013) pia alibaini kwamba wazungumzaji wa lugha ya Kikuyu walichanganya sauti /l/ na /r/ walipokuwa wakiandika ufahamu katika lugha ya Kiswahili. Kulingana nae, sehemu ambapo sauti / r / ilipaswa kutumika, sauti / l / ilitumika badala yake. Kulingana na nadharia ya Uchanganuzi Dosari wajifunzaji wa lugha ya pili hupata ugumu wa kutumia baadhi ya sauti ya lugha wanayojifunza, na hivyo kulazimika kutumia sauti nyingine mbadala. Katika mazingira ya namna hii, dosari kwa wajifunzaji wa lugha ya pili haziwezi kuepukika.

#### 4.1.3 Dosari za Udondoshaji wa Sauti

Utafiti pia ulibaini kwamba wanafunzi walifanya dosari zilizohusu udondoshaji wa vipashio, silabi au viambishi wakati wakitamka maneno ya lugha ya Kiswahili. Udondoshaji ni hali ya kuondoa kipashio cha kiisimu katika maneno au sentensi, na hivyo kukiuka taratibu za lugha husika. Massamba (2016) anaeleza kuwa udondoshaji sauti ni uondoaji, ama kwa makusudi au kwa bahati mbaya, wa sauti moja au mbili katika neno. Tatizo la udondoshaji lilijitokeza katika matamshi ya wanafunzi wa jamii ya Kingoni. Aidha, mfano wa dosari zilizohusu udondoshaji wa sauti ni kama zinavyodhihirishwa katika Jedwali Na. 1.7 hapa chini:

**Jedwali Na. 1.7: Dosari za Udondoshaji wa sauti /h/**

Na.	Dosari	Kiswahili Sanifu
a)	<i>akuna</i>	<i>hakuna</i>
b)	<i>alufu</i>	<i>harufu</i>

c)	<i>asubui</i>	<i>asubuhi</i>
d)	<i>mualule</i>	<i>mhalule</i>

**Chanzo:** Data za Uwandani

Katika data Na. 1.7. (a)- (d), ni dhahiri kwamba udondoshaji wa kitamkwa /h/ unafanywa pale ambapo kitamkwa hicho kinatanguliwa na sauti /a/ au kinafuatiwa nasauti /e/. Aidha, tofauti na sauti nyingine za konsonanti ambazo zinakuwa na mbadala wake wakati wa utamkaji, fonimu /h/ haina sauti nyingine iliyo na ukuruba wa kifonetiki nayo, ambayo inaweza kuchukua nafasi yake. Hali hii inafanya kitamkwa /h/ kudondoshwa katika mazingira yoyote inapojitokeza. Hata hivyo, Ontieri (2013) katika utafiti wake alibaini wazungumzaji wengi wa lugha za kibantu za Kenya walidondosha sauti / m/ na /n/ na / h/ walipokuwa wakijifunza au kuzungumza lugha ya Kiswahili ikiwa ni lugha yao ya pili. Kulingana na Nadharia ya Uchanganuzi Dosari, hatua ya pili ya uainishaji na uchambuzi wa data ambayo inahusu ubainishaji wa dosari zilizochambuliwa imehitimishwa.

## 5.0 Hitimisho na Mapendekezo

Kwa kuhitimisha, dosari za kifonolojia kwa Wangoni wapapojifunza Kiswahili wilaya ya Songea zimejadiliwa. Sababu kubwa zilizokulia dosari hizo ni miundo tofauti kati ya lugha ya Kingoni na Kiswahili. Dosari hizo zinaleta athari si tu katika mawasiliano na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, bali pia hata kuathiri ufaulu wa wanafunzi shuleni. Ili kutatua chanzo kikuu cha dosari hizo watunga mitaala pamoja na wadau wa elimu nchini wanapaswa kuandaa mitaala pamoja na kanuni za ufundishaji wa umahiri wa lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia jamiilugha za Kibantu. Hatua hii itasaidia kutatua changamoto zinazosababisha dosari kwa wanajamii wa lugha za Kibantu wanapojifunza au kuzungumza Kiswahili licha ya kuwa ni lugha yao ya pili.

Kadhalika, utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa katika uwanja wa isimu pamoja na wadau mbalimbali wa Kiswahili na watafiti. Kwanza, utafiti huu utachagiza watafiti wengine kushughulikia dosari za viwango vingine katika lugha nyingine za Kibantu hususani wanapochunguza dosari katika lugha ya pili au lugha za kigeni. Hata hivyo, utafiti huu haukushughulikia dosari zote zinazowakumba wanafunzi wa jamii ya Kingoni wanapozungumza lugha ya Kiswahili. Hivyo, tunapendekeza dosari za vipengele vingine vya kiisimu nje ya fonolojia zichunguzwe ili matokeo yatakayopatikana yaweze kulinganishwa na utafiti huu na kubainisha dosari katika viwango vingine.

### Marejeleo

- Al- Shuabi, M. A. (2006). Phonological Analysis of English Phonotactics of Syllable Initial and Final Consonant Clusters by Yemen Speakers of English. Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Science, Malaysia.
- Amro, M. E. E. (2013). The pronunciation Errors of L1 Arabic learners of L2 English. The Role of modern standard Arabic and Vernacular Dialects Transfer. Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha British, Dubai..
- Arnaud, B. (2015). Errors Anaalysis as a remedy for pronunciation problems; The case of Tanzanians students learning French. Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Tlemcen.
- Badawi, K. (2012). An Analytic of Phonetic, Morphological and Syntactic errors in English. A case study of Saudi BA students. Tasnifu ya MA. Chuo Kikuu cha King Khalid.
- Brown, H. D. (1994). *Principles of Language Learning and Teaching* (Toleo la 3), New York: Prentice Hall.
- Corder, S. P. (1967). *Error Analysis and Interlanguage*, Oxford: Oxford University Press.
- Dulay, H. na Burt, M. (1974). *Natural Sequence in Child Second Language Acquisition*. Language Learning, Juzuu 24, 23-40.
- Gawasike, A. (2016). Ukakamaaji wa Wajifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika Jamii ya Wakinga. Tasnifu ya Uzamivu. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu chaDar es Salaam.
- Kisakwah, B. A. (2014). Uchanganuzi Dosari na Muundo Sentensi: Ulinganisho wa Sentensi Sahili za Kiswahili Sanifu na za Kisuba. Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age Internation Publishers.
- Lado, R. (1957). *Linguistics Across Cultures: Applied Linguistics for Language Teachers*. Ann Arbor, MI, US: University of Michigan Press.
- Mangwa, D. O. (2005). Athari za Kikisii katika Kiswahili na Zinavyochangia Matokeo Mabaya ya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili kwa Wanafunzi Wakisii Wilayani Kisii Kusini. Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Massamba, D. P. B. (2016). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbula, E. J. (2011). Dosari za Kifonolojia Zinazofanywa na Wazungumzaji wa Kikamba Wanapozungumza Lugha ya Kiswahili. Tasnifu ya M.A.

- (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Msigwa, A. B. G & Vavayo, A. S. ( 2020). Aina za Dosari za Kifonolojia Zinazojidhihirisha kwa Wajifunzaji Wajifunzaji wa Kiswahili katika jamii ya Wamaasai. Jarida la CHALUFAKITA 2020. Juz. Na. 2
- Mudhune, D. R.. (2008). Athari za Kifonolojia kwa Wasemaji wa Dholuo Wanaojifunza Kiswahili. Tasnifu ya M. A. (Haijachapwa) Chuo Kikuu cha Egerton.
- Nyanda, J. (2015). Athari ya Lugha ya Kinyamwezi katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili. Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa) Chuo Kikuu Huria Tanzania.
- Obara, J. M. (2014). Uchanganuzi wa Makosa yanayofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii nchini Kenya. Tasnifu ya M.A (Haijachapwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Ontieri, J. O. (2013). Phonological Influences of First Language on Kiswahili: A Case Study of Kenyan Bantu Languages. *International Journal of Science and Research*, 2, 2523-2526. <https://shorturl.at/YDLOx>
- Otiende, M. A. (2013). *Athari za kimofofonolojia za kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama lugha ya pili*. Doctoral Dissertation, University of Nairobi. <http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/59341>.
- Virginia, V.W. (2016). Dosari za Kifonolojia Zinazofanywa na Wazungumzaji wa Lahaja ya Kiamu na Kitikuu katika Kujifunza Kiswahili Sanifu. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.